TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA
Kitalu Na. 8, Mtaa wa Luthuli
S.L.P 2643, DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2135747/8; 2137125; 2135222
Faksi: +255 22 2111281
Barua Pepe: chragg@chragg.go.tz
Tovuti: www.chragg.go.tz

Aprili 25, 2015

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## Mapendekezo ya Wadau Kukomesha Ukatili dhidi ya Watu wenye Ualbino

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) hivi karibuni ilikutana na wadau mbalimbali wa haki za binadamu ili kujadili mikakati ya kukomesha ukatili na mauaji yanayoendelea dhidi ya watu wenye ualbino.

Washiriki katika mkutano huo walitoka kwenye taasisi za Serikali, asasi za kiraia vikiwemo vyama vya watu wenye ualbino na taasisi za kidini. Wajumbe wengine walitoka kwenye mashirika ya Umoja wa Mataifa hapa nchini.

Katika mkutano huo wadau wote kwa pamoja walikemea mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino, unaofanywa na watu wenye imani za kishirikina, ambao wanaamini kuwa utajiri na vyeo au madaraka ya kisiasa vinapatikana kupitia matumizi ya viungo vya watu wenye ualbino.

Aidha, walikubaliana kuwa mapambano dhidi ya ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino ni suala mtambuka linalohitaji rasilimali fedha za kutosha, pia jitihada za pamoja ili kufanikiwa.

Hivyo wadau wanaiomba Serikali kutenga fedha za kutosha kwa taasisi zote za Serikali zinazohusika na suala hili kwa ajili ya kutekeleza programu za kuelimisha umma, kuharakisha upelelezi na uendeshaji wa kesi za watu wanaodaiwa kufanya ukatili na mauaji dhidi ya watu wenye ualbino.

Pia wameiomba jumuiya ya kimataifa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Tanzania katika mapambano yake dhidi ya ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino nchini kwa kuipatia fedha na misaada ya kiufundi.

Mapendekezo mengine muhimu ya namna ya kukomesha ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino, yakiwemo yaliyomo humu, yaliainisha wajibu wa kila mdau, kama ifuatavyo:

1. **Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

   Kwa kushirikiana na wadau wengine, iandae mswada wa marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Uchawi, Sura ya 18 hususan Kifungu cha 8(1) kinachompa Mkuu wa Wilaya mamlaka ya kumhamisha mtu anayehisiwa kwa uchawi kwenda sehemu nyingine. Inapendekezwa kuwa kifungu hiki kirekebishwe ili washukiwa hao washtakiwe mara baada ya Jeshi la Polisi kukamilisha upelelezi wake.

   Kwa kushirikiana na wadau wengine, iandae mswada wa marekebisho ya Sheria ya Tiba Asilia na Mbadala ya mwaka 2001 kwa kuangalia hususan maana ya dawa tiba mbadala na kufuta vifungu vinavyoruhusu matumizi ya viungo vya wanyama katika dawa tiba mbadala.

2. **Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP)**

   Iainishe masuala ya mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa ya mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino na kuyapa kipaumbele katika kuyashughulikia.

3. **Idara ya Mahakama**

   Iharakishe usikilizaji wa mashauri ya mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino na kutoa hukumu kwa wakati ili kulinda haki za kundi hilo.

4. **Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

   Kwa kushirikiana na wadau wengine, iandae Programu endelevu wa kutoa elimu kwa umma juu ya haki za binadamu hususan ulinzi na utetezi wa haki za watu wenye ualbino.

   Iratibu na kutekeleza Programu hiyo ili hatimaye jamii itambue kuwa mtu mwenye ualbino ni mtu wa kawaida kama walivyo binadamu wengine na hivyo anastahili haki zote. Anachopungukiwa yeye ni vinasaba vya *melanin* ambavyo huchangia kutoa rangi nyeusi kwenye ngozi ya kila binadamu. Elimu hii isambazwe kuanzia shule za msingi hadi vyuo vya elimu ya juu, pia vijijini na mijini.

5. **Idara ya Uhamiaji**

   Isimamie kikamilifu utekelezaji wa Sheria za Hamiaji. Iwabaini waganga wa jadi kutoka nje ya nchi wanaokuja na kufikia nyumba za kulala wageni hapa nchini na kuendesha shughuli zao kinyume na taratibu.

6. **Jeshi la Polisi**
   Kwa kushirikiana na wadau wengine, lifanye uchunguzi na upelelezi wa kina kubaini mtandao wa wanaohusika na mauaji ya watu wenye ualbino wakiwemo waganga wa jadi, wanunuzi, wakataji na watumiaji wakuu wa viungo vya watu wenye ualbino.

   Kwa kushirikiana na Ofisi ya DPP wakamilishe mapema upelelezi wa kesi za ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino ili mahakama zisikilize kesi hizo haraka na kuzitolea maamuzi ya haki.

   Litoe vibali vya mikutano kwa viongozi wa dini kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo ili kuwawezesha kufanya kazi ya uenezaji dini na kutoa ushauri na miongozo ya kiroho.

7. **Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**
   Ianzishe vitengo maalumu katika hospitali na vituo vya afya katika ngazi ya Wilaya na Mkoa kwa ajili ya uchunguzi wa mapema na tiba ya magonjwa ya ngozi na magonjwa mengine yanayowaathiri watu wenye ualbino, kwa kuwa hivi sasa tiba ya saratani ya ngozi inapatikana katika Hospitali za Rufaa tu.

   Itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mafuta ya kuzuia athari za ngozi, miwani na kofia kwa watu wenye ualbino na kuvisambaza katika vituo vyote vya afya kuanzia mkoani hadi vijijini. Nao wavitoe kwa wahusika bure.

   Kupitia Msajili wa Baraza la Waganga wa Tiba Asilia na Tiba Mbadala ifanye uhakiki wa waganga wanaofanya kazi bila vibali na kuwafungia. Aidha, ikishirikiana na Jeshi la Polisi, ipeleleze na kuwabaini wanaofanyakazi kinyume na maadili ya kazi zao na kuwafutia leseni.

   Idhibiti matangazo ya waganga wa jadi yanayobandikwa kiholela mitaani na kwingineko kwani yanachangia kuendeleza utamaduni wa imani za kishirikina.

8. **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**
   Shule za watoto wenye mahitaji maalumu ziongezwe na kupatiwa walimu wenye taaluma husika na vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia.

   Ili kuongeza uelewa wa masuala haki za binadamu na watu wenye ualbino Wizara ihakikishe kuwa inayaingiza masuala hayo katika mitaala ya mafunzo.

   Inapaswa kujitahidi kutekeleza kikamilifu elimu jumuishi kwa watoto wenye ualbino.

**9. Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)**

Ziimarishe ulinzi wa watu wenye ualbino kwa kupitia kamati za ulinzi na usalama za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji zikishirikiana na ofisi za Ustawi wa Jamii. Ulinzi huo uanzie katika ngazi ya kaya hadi taifa na kwamba kamati hizi zielimishwe jukumu hili.

Kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Takwimu *(National Bureau of Statistics)* iweke mfumo wa kisensa wa kutambua watu wenye ualbino katika ngazi zote. Takwimu hizi wapewe Jeshi la Polisi ili ziwasaidia kuhakikisha kuwa watu wenye ualbino wanalindwa kikamilifu.

**10. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo**

Ihamasishe vyombo vya habari, hususan radio za jamii katika kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na wajibu wa jamii katika kutambua na kuheshimu haki za watu wenye ualbino.

**11. Asasi za Kiraia**

Zishirikiane na THBUB na wadua wengine katika kuandaa na kutekeleza mipango endelevu ya kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na wajibu wa jamii hususan katika kutambua na kuheshimu haki za watu wenye ualbino.

**12. Madhehebu ya Dini**

Viongozi wa dini zote waendelee kutoa ushauri na mafundisho ya kiroho yenye lengo la kujenga jamii inayoheshimu, kupenda na kuthamini haki na utu wa mtu, hususan haki za watu wenye ualbino.

Mapendekezo haya yanalenga kutoa ulinzi na huduma za afya kwa watu wote wenye ualbino nchini. Ushiriki wa jamii katika ngazi zote ni muhimu katika kupata mafanikio katika suala hili.

Kwa niaba ya wadau wote, Tume inatoa wito kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika kuhakikisha kuwa mapendekezo haya yanatekelezwa.

Tume inapenda kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kukemea au kuchukua hatua mahsusi za kupambana na mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino, na kuwasaidi wahanga na watu wenye ualbino kwa ujumla.

Imetolewa na:

Mhe. Bahame Tom Mukirya Nyanduga
**Mwenyekiti**

Aprili 25, 2015